



TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe anawatangazia uwepo wa nafasi za kazi kwa Ajira ya Mkataba wa Kujitolea. Nafasi hizo zinahusu kada zifuatazo: Maafisa Wauguzi Wasaidizi (ANO), nafasi kumi na nne (14), Wasaidizi wa Afya (MATT) nafasi kumi (10), Dereva, nafasi moja (1), na Afisa Habari nafasi moja (1).

Watanzania wenye sifa ya kuomba, na kujaza nafasi hizi, wanaombwa kuleta maombi ya:

1. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI

Mwombaji awe na stashahada ya Uuguzi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, vyeti vya Uuguzi na Ukunga na leseni hai.

2. MSAIDIZI WA AFYA

Mwombaji awe na cheti kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali,

3. DEREVA

Mwombaji awe na cheti kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na leseni hai.

4. AFISA HABARI

Mwombaji awe na stashahada au shahada kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali

SIFA ZA JUMLA

1. Awe na umri usiozidi miaka 35 (Thelathini na tano)
2. Awe amefaulu kidato cha Nne / Sita
3. Awe na kitambulisho cha Uraia na
4. Awe na wadhamini wawili wanaotambulika na Serikali ya Kijiji/ Mtaa

anapoishi.

MASHARTI YA JUMLA

Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kidato cha Nne / Sita, cheti cha taaluma, cheti cha kuzaliwa, maelezo binafsi (curriculum Vitae).

Waombaji watakaowasilisha "*Result Slip*", "*Statement of Result*", "*Provisional Result*" au "*Transcript*" **HAWATAKUBALIWA.**

Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe,
S.L.P 910.

DODOMA

Au kupitia barua pepe: barua@mirembe.or.tz

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 08 Aprili, 2026, Saa **9:30 Alasiri.**

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MTENDAJI
HOSPITALI YA TAIFA YA AFYA YA AKILI MIREMBE**

20/03/2026